

# Umbali wa Sala Tu

Prodi alikuwa mwoگا kurudi kulala. Vipi ikiwa angepata ndoto nyingine ya kutisha?



VIELELEZO NA KATIE PAYNE

**Na Lucy Stevenson**  
Majarida ya Kanisa

*“Sali, Yeye yupo”*  
(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 12).

**P**rodi aliketi kitandani kwa mshtuko. Moyo wake ulikuwa ukidunda kwa kasi.

Mvua ilinyesha kwa vishindo vidogo vidogo juu ya paa wakati alipokuwa ameketi gizani. Aliweza kusikia maji yakidondoka kutoka kwenye mtini wa Kiafrika nje ya dirisha lake, na hewa ilikuwa nzito na yenye joto. Prodi alivuta pumzi ndefu na kujaribu kutulia. Ilikuwa ni ndoto tu.

Alitambaa kutoka kitandani na kuchungulia chumbani kwa wazazi wake. Mama na baba walikuwa wamelala kwa utulivu. Dada yake mdogo, Célia, alikuwa amejikunjia ndani ya kitanda chake pia. Kila kitu kilikuwa SAWA. Familia yake ilikuwa salama.

Prodi alirudi kitandani na kujaribu kusinzia tena. Alijirusha na kugeuka, kisha kujirusha na kugeuka tena na tena. Alijua ndoto yake haikuwa kweli, lakini ilikuwa ya kuogopesha! Japokuwa alikuwa amechoka, aliogopa kusinzia tena. Vipi ikiwa angepata ndoto nyingine ya kutisha?

Prodi alilala chali na kutazama dari. Alijaribu kufikiria mawazo ya furaha. “Baba wa Mbinguni, je, kweli upo? Na je, unasikia na kujibu sala ya kila mtoto?” Wimbi la upepo lilikuja juu ya Prodi wakati alipofikiria maneno ya wimbo wake alioupenda sana wa msingi. Dada Kioska alikuwa amewafundisha kwamba Baba wa Mbinguni



daima alikuwa akiwalinda. Wangeweza kusali kwake wakati wowote, mahala popote. Prodi alijua nini cha kufanya. Alishuka kitandani na kupiga magoti ili kusali.

“Baba mpendwa wa Mbinguni,” alisali,

“ninaogopa sana. Tafadhali iweke salama familia yangu. Na tafadhali nisaidie nipate usingizi na nisipate tena ndoto mbaya.”

Prodi alimaliza sala yake na kurudi kitandani. Mwili wake ulitulia, na akili yake ilihisi amani. Punde alisinzia.

Kulipokucha asubuhi, Prodi aliamshwa na jua lenye joto lililong’ara kupitia dirishani. Aliweza kusikia masufuria yakigongana jikoni na aliamka kumtafuta Mama. Célia alikuwa mezani akila kiporo cha mihogo. Mama alikuwa akipasha mihogo mingine kwa ajili yake pia.

“Habari ya asubuhi,” Mama alisema. “Ulilalaje?”

“Nilikuwa na ndoto ya kutisha,” Prodi alisema. “Lakini kisha nikasali. Baba wa Mbinguni alinisaidia kuhisi salama.”

“Pole kwa kuwa na ndoto mbaya,” Mama alisema. Alimkumbatia Prodi kwa muda mrefu. “Lakini ninafurahi ulisali. Inaonekana kama vile Baba wa Mbinguni kweli alikusaidia.”

“Ni kweli,” alisema Prodi. “Niliweza kusinzia tena, na sikuwa tena na ndoto mbaya.” Prodi alimkumbatia Mama kwa nguvu. Alikuwa na furaha kujua kwamba licha ya woga aliohisi, Baba wa Mbinguni alikuwa umbali wa sala tu. ●

**Funua ukurasa kukutana na mvulana kutoka kwenye hadithi hii!**